# Matumizi ya Anagramu, Kanuni ya Rebasi, Seti, Emoji na Akronimi kama Mitindo ya Sanaa ya Uandishi

*Benard Odoyo Okal**

**Ikisiri**

*Sanaa ya uandishi imeendelea kutokea katika mfumo wa kikabari, kihiroglifu, kilogografu, kisilabi, na kialfabeti. Imebainika kuwa tunapoendelea kimaandishi kutoka mfumo mmoja tunaelekea kuhama pia na vipashio vingine vya mifumo ya awali. Hivyo basi, chembechembe za mifumo ya awali zingali zinadhihirika katika mitindo mingine ya kisasa ya matumizi ya lugha kama tunavyoona katika rebasi, seti, na emoji. Kwa hiyo, makala haya yanalenga kufafanua mitindo ya rebasi, seti na emoji, pamoja na anagramu na akronimi kama sanaa ya uandishi ili kutambua ishara zinazotumiwa na zilizokubaliwa katika lugha. Makala yanahusisha dhana, dhima, historia, na maendeleo ya sanaa ya uandishi. Yanaonyesha pia jinsi mitindo ya anagramu, rebasi, seti, emoji, na akronimi inavyodhihirika kama sanaa ya uandishi. Data zilikusanywa maktabani kwa kutumia upekuzi, kuteuliwa kidhamirifu na kuchanganuliwa kimaudhui.*

**Dhana za msingi:** *uandishi, anagramu, rebasi, seti, emoji na akronimi*

**Abstract**

*The art of writing has systematically developed from cuneiform, hieroglyphic, logographic, syllabic to alphabetic writing. However, it has emerged that as we develop writing from one system to the other we also tend to carry along some aspects of the earlier systems. Hence, some elements of the early writing systems tend to be present even in the current writing systems as witnessed in the use of rebus, set and emoji. This article, therefore, intends to explain how the rebus, set, emoji, and also anagram and acronym styles are used as forms of writing in language. The article involves the concept, functions, history and development of art of writing in its scope. It also shows how anagram, rebus, set, emoji and acronym styles manifest themselves as forms of writing. Data was collected by the use of observation from the library, purposively sampled and analysed thematically.*

**Keywords:** *writing, anagram, rebus, set, emoji and acronym*

*Mhadhiri, Idara ya Kiswahili na Lugha nyingine za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Maseno, S.L.P. 333, Maseno, Kenya, Barua pepe: benardodoyo@yahoo.com

**Utangulizi**

Uandishi ni mfumo maalum wa kuwakilisha usemi au matumizi ya ishara zilizobuniwa na zinazoweza kutambulika pamoja na vitu vingine vinavyotumiwa kuwasiliana (Gelb, 1963; Olson, 2009). Ishara hizi huunda seti maalum na huweza kuonekana na kutambuliwa na jamiilugha husika (Cheng, h.t.). Uandishi hurejelewa pia kama lugha iliyoandikwa; mbinu au mifumo yoyote ya ishara inayotumiwa kuwakilisha lugha na ambayo hudhihirika kama mwandiko, upigaji chapa na uwasilishaji wa kielektroniki (Fromkin, Rodman & Hyams, 2007).

Hivyo basi, uandishi ni kazi maalum ya kuandika (TATAKI, 2013). Kile kinachoandikwa aghalabu huwa alama au ishara za kuwakilisha vipashio vya lugha semwa na vinavyoweza kuwekwa kwenye vifaa kama vile karatasi, chuma, na udongo (Thompson, 2016). Kwa kuwa sanaa ni ufundi maalum wa kuwasilisha hisia pamoja na mawazo ya binadamu katika maandishi, michoro, nyimbo au uchongaji (TATAKI, 2013), basi sanaa ya uandishi ni ufundi wa kuwasilisha hisia na mawazo mengine kimaandishi.

Japo maendeleo ya sanaa ya uandishi yamepitia mifumo ya kikabari, kihiroglifu, kilogografu, kisilabi na kialfabeti, baadhi ya masuala yaliyozingatiwa katika mifumo hii ya kizamani yangali yanadhihirika katika maandishi ya kisasa. Kwa mfano, ishara zisizo za kialfabeti zingali zinatumiwa kama tunavyoona katika mitindo ya kanuni ya rebasi, seti na emoji. Hali hii hudhihirisha kuwa, japo sanaa ya uandishi inazidi kuimarika, kuna chembechembe za mifumo ya uandishi wa kizamani ambazo zingali zinatumiwa katika maandishi ya kisasa ya kialfabeti. Hivyo basi, mbali na ishara za kialfabeti au kifoniki zinazozingatiwa katika mfumo wa kialfabeti, pia kuna ishara nyingine zisizo za kialfabeti zinazotumiwa kama tunavyoona katika taaluma ya hisabati na sayansi (Gelb, 1963) na hata isimu, hasa isimu kihisabati. Ishara hizo pia hudhihirisha matumizi ya sanaa ya uandishi.

Maelezo hayo huchangia hali kuwa sanaa ya uandishi huweza kuchukua njia mbili za uwakilishaji kama vile ya kisenemiki (cenemic) na kipleremiki (pleremic) (Baroni, 2011). Senemiki hurejelea vipashio vile vinavyosimamia foniki, yaani herufi fulani husimamia sauti husika. Pleremiki huangazia vipashio kama vile picha au alama nyingine bunifu zinazotumiwa kusimamia jambo kama tunavyoona

katika mifumo ya pichataarifa na wazotaarifa. Njia hizi mbili huingiliana na kuchangiana.

Hivyo basi, makala haya yanaonyesha namna tunavyoweza kutumia ishara za kialfabeti na zisizo za kialfabeti katika mitindo teule ya sanaa ya uandishi kama vile anagramu, rebasi, seti, emoji, na akronimi. Ili kujenga na kuimarisha upeo na ufafanuzi wa makala haya, vipashio vifuatavyo vimezingatiwa: historia, maendeleo, na dhima za sanaa ya uandishi. Pia kuna fafanuzi za mitindo mbalimbali ya sanaa ya uandishi kama vile anagramu, kanuni ya rebasi, nadharia ya seti, emoji, na akronimi.

Makala yamejengwa kwa kuzingatia muundo elezi ambapo masuala husika yameelezwa kinathari. Data zilikusanywa maktabani kutoka makala mbalimbali za kiisimu kwa kutumia mbinu ya upekuzi. Data husika ziliteuliwa kidhamirifu ili kukidhi matakwa ya mada hii. Usampulishaji dhamirifu ulizingatiwa katika utoaji wa mifano mwafaka. Data zilichanganuliwa kimaudhui kama vile anagramu, kanuni ya rebasi, nadharia ya seti, emoji, na akronimi. Data zilizorejelewa zimewasilishwa kinathari na kwa kutumia vielelezo mwafaka kama vile michoro, alama, na picha maalum.

## Historia na Maendeleo ya Sanaa ya Uandishi

Chimbuko la sanaa ya uandishi hufafanuliwa kwa nadharia mbalimbali kinzani kama lilivyo chimbuko la lugha kwa ujumla. Utata huu wa chimbuko la lugha huchangia kuwepo kwa makundi mawili ya nadharia, kama vile nadharia ya kiasilia na kiulezi (Amanda, 2015). Nadharia ya kiasilia hutokana na maoni ya Darwin aliyechunguza chimbuko la lugha kwa kuangazia mifumo ya mawasiliano ya wanyama katika mazingira asilia. Nadharia ya kiulezi huchunguza lugha kama mali ya binadamu bila kuihusisha na sauti za wanyama. Hata hivyo, kuna nadharia mahususi zinazoweza kutumiwa kufafanua chimbuko la lugha kama vile nadharia ya mama, bow-bow, pooh-pooh, ding-dong na woo-woo (Amanda, 2015; Mentalfloss, 2016; Sprunger, h.t.; TUKI, 1990).

Utata wa chimbuko la lugha hutupa msingi wa kung'amua kuwa chimbuko la sanaa ya uandishi pia huwa tata na linahusisha nadharia nyingi kinzani. Hii ni kwa sababu lugha kama mfumo wa mawasiliano hujumuisha masuala mawili; ambayo usemi na uandishi kama yanavyotumiwa na wanajamii katika mazingira yao maalum (Hornby, 2010). Hivyo basi, ni jambo la busara kujua chimbuko la lugha kwa

sababu lugha husemwa na yale yaliyosemwa huandikwa ili kuyahifadhi. Aidha, chimbuko la lugha hutusaidia kung'amua kuwa binadamu aghalabu hujua kusema lugha husika kabla ya kujua kuiandika kwa kutumia mifumo mbalimbali (Yule, 1996). Chimbuko la sanaa ya uandishi linaweza kuelezwa kwa mitazamo anuwai. The Huntington (h.t.), Gelb (1963) na Fromkin na wenzie (2007) wanabainisha mitazamo ifuatayo kama inavyofafanuliwa katika aya zinazofuata:

Kwanza, sanaa ya uandishi ilitokana na ngano maalum. Mathalani, Cadmus (mwana wa mfalme wa Foenisi) anaelezwa katika ngano ya Kigiriki kuwa ndiye mvumbuzi wa alfabeti na kuileta huko Ugiriki. Katika jamii ya watu wa Ayalandi kuna ngano kuhusu Ogmios aliyekuwa mvumbuzi wa uandishi. Katika kisasili cha Babilonia palikuwepo na miungu wawili; Nebo au Nabu (mlezi wa sayansi) na Thoth kutoka Misri aliyevumbua mfumo wa kihiroglifu. Katika hekaya za Kichina kulikuwepo na miungu wawili; Cang Jie (Ts'ang Chien) na Fohi iliyovumbua sanaa ya uandishi. Vilevile msomi mmoja aitwaye Rabbi Akiba kutoka Talmudic aliamini kuwa alfabeti zilikuwepo hata kabla ya binadamu kuumbwa; hivyo basi, ni jambo lililotokea kiasilia.

Pili, uandishi ulitokana na masuala ya kidini na imani. Katika Uislamu, alfabeti ziliumbwa na Allah aliyewapa binadamu kuzitumia katika shughuli zake huku akitumia kalamu ya mafunjo. Waebrania nao waliamini kuwa sanaa ya uandishi ililetwa na Mungu kama tunavyoona katika kitabu cha *Kutoka* 31:18:

> Hapo BWANA alipokuwa amekwisha zungumza na Musa katika Mlima Sinai, akampa hizo mbao mbili za ushuhuda, mbao mbili za mawe, zilizoandikwa kwa chanda cha Mungu (Bible Society of Kenya, 1997:92).

Baadaye binadamu akaanza kuandika mwenyewe kwa mikono yake kama tunavyodhihirishiwa katika kitabu cha *Isaya* 8:1:

> BWANA akaniambia, ujipatie ubao mkubwa ukaandike juu yake kwa kalamu ya binadamu... (Bible Society of Kenya, 1997:741).

Kule Liberia na Gine, mhusika Wido ndiye alivumbua uandishi. Mtu huyu alikuwa na ilhamu kutoka kwa Mungu kuwa katika nchi hizo mbili jamii au kabila la watu lililojulikana kama Toma lilipewa uwezo wa kuandika; hata hivyo, walionywa wasiwaeleze wanawake wao.

Haijulikani kwa nini Wido alitahadharishwa hivyo. Hata hivyo, tunaweza kubashiri tu kwamba huenda jamii hiyo ilizingatia mno mfumo wa kiubabedume ambapo wanawake walionekana kama watu wa tabaka la chini lisilo na hadhi na pia watu wasioweza kuficha kunga maalum.

Tatu, kwa mujibu wa jamii ya Wahindi, Brahma ndiye alimpa binadamu maarifa ya herufi ambazo zilitumiwa kama msingi wa sanaa ya uandishi. Kimsingi, Brahma hurejelewa kama mhindi wa tabaka la juu.

**Uvumbuzi wa Sanaa ya Uandishi**

Ingawa kuna ngano na maelezo mengine kuhusu chimbuko la sanaa ya uandishi, ni jambo linalokubaliwa kuwa uvumbuzi wa uandishi ulianza kuonekana baada ya binadamu kujua kuzungumza na uvumbuzi huo ulipitia hatua mbalimbali (Fromkin na wenzie, 2007). Kilichochangia uvumbuzi wa sanaa ya uandishi ni kuwa binadamu alizoea kukusanya matunda na nafaka, kuwinda na kulima ili kukidhia mahitaji yake. Hivyo basi, wanajamii waliweza kupata mazao na bidhaa tele katika mazingira yao.

Kutokana na hali hii, binadamu alianza kustaarabika. Hivyo basi, pakatokea haja ya kurekodi vitu vyao na haja hiyo ikachangia uvumbuzi wa uandishi (Kasprowics, 2011). Baadaye binadamu alianza kujiundia picha zilizoashiria suala maalum kwa kutumia alama kama vile nukta, mistari, na ishara nyingine dhahania. Picha hizi zilichorwa katika mapango kama zile zilizoonekana kule Perch Merle na Lascaux ya kule Ufaransa kati ya miaka 30, 000 na 17, 000 iliyopita (Kasprowics, 2011).

Picha hizi dhahania (picha ambazo hazikuhusiana kamwe na kile kilichorejelewa) ziliimarishwa na kuzalisha picha zilizowakilisha ujumbe fulani. Baadaye watu wakaanza kuhusisha ishara zilizotolewa na sauti zilizotamkwa na binadamu mradi tu ishara hizo zilipoonekana. Picha hizi ziliwekwa au kupangwa kwa kufuatana, kuhusishwa na sauti, na kuwakilisha neno au maneno maalum yaliyotamkwa.

Ishara za sanaa ya uandishi ya awali zilikuwa michoro iliyochorwa kwenye mapango maalum. Michoro yenyewe ilirejelewa kwa jina maalum kama petroglifu na ilichorwa na binadamu zaidi ya miaka elfu ishirini iliyopita (Fromkin na wenzie, 2007). Baadaye, sanaa ya

uandishi ikaanza kuimarika na hatimaye kujitokeza mifumo miwili ya uandishi wa awali; pichataarifa na wazotaarifa (Fromkin na wenzie, 2007; Yule, 1996).

Pichataarifa humaanisha matumizi ya ishara au picha maalum ya kuwakilisha taarifa fulani. Ishara au picha hizi zilipoendelea kutumika na kukubaliwa na watumiaji wa lugha husika, basi uandishi wa pichataarifa ukaimarika. Kila ishara katika pichataarifa hufaa kuwa na maana moja tu la sivyo fasiri nyingi huhinikiza mawasiliano (Falck, 2001). Ingawa mfumo huu ulidhihirika katika ulimwengu wa zamani, ungali unatumika sasa katika alama za barabarani, mbuga za wanyama, misalani na kadhalika. Tazama mfano wa pichataarifa ambapo ishara 1 humaanisha binadamu wa kiume. Ishara hii aghalabu hubandikwa langoni mwa msala ili kuwaelekeza wanaume:


1

Wazotaarifa au idiogramu hurejelea ishara zile za kimaandishi zilizotumiwa kuwakilisha wazo fulani katika mazingira husika (Knight, 2009). Mathalani, ingawa kinyota kilitumiwa kuashiria jua, kilielekea kutumiwa pia kuashiria mawazo mengine mengi dhahania kama vile joto, mwangaza, fufutende, na ishara ya mchana. Ishara hizi aghalabu huwakilisha vifaa na dhana zinazohisika tu (Rebus Game, h.t.; Linguistics 203, h.t.).


Kwa jumla, maandishi ya awali aghalabu yaliwekwa kwenye vipande vya udongo wenye majimaji uliofinyangwa na yalihusu idadi ya watu na vitu kama vilivyoonekana kule Mesopotamia katika Milenia ya 9 KK (Olson, 2009). Baadhi ya malighafi zilizotumiwa zilikuwa mawe, udongo, mafunjo, mifupa ya wanyama, maganda ya miti na pia ngozi za wanyama (Kasprowics, 2011).

**Mifumo mingine ya Sanaa ya Uandishi**

Baada ya mifumo tangulizi ya sanaa ya uandishi hasa pichataarifa na wazotaarifa kuimarika, mifumo mingine mbalimbali ilianza kuonekana baadaye miongoni mwa jamii na katika maeneo mbalimbali ulimwenguni. Hivyo basi, maendeleo ya sanaa ya uandishi yanaweza kugawanywa katika mifumo mbalimbali kuanzia mfumo wa kikabari, kihiroglifu, kilogografu, kisilabi, na kialfabeti (Fromkin na wenzie, 2007; Gelb, 1963; Knight, 2009; Lingusitic 203, h.t.; Yule, 1996):

**Mfumo wa Kikabari**

Katika mfumo huu, ishara ziliandikwa kwenye udongo wa mfinyanzi kwa kutumia sindano kama ya santuri iliyokuwa na mdomo uliokuwa na umbo la kabari au chembeo (Fromkin na wenzie, 2007). Hivyo basi, binadamu alianza kutumia ishara ili kurejelea jina maalum la kifaa badala ya kifaa chenyewe. Sindano ya santuri yenye umbo la kabari ilifinywa kwenye udongo wenye majimaji ili kujitokeza ishara fulani iliyoweza kutambuliwa na wasemaji wa lugha husika. Mfumo huu ulitumika aghalabu kule Sumeria hasa katika ustaarabu wa Mesopotamia (Iraki) (Olson, 2009). Mfumo huu ulidhihirika miaka 6,000 iliyopita na baadaye kusambaa hadi Mashariki ya Kati, Asia, Uajemi, Assyria na hata Babilonia (Fromkin na wenzie, 2007). Ishara kama ifuatayo ilitumiwa kuwakilisha neno 'samaki' kwa msingi wa mfumo wa kikabari (Fromkin na wenzie, 2007:508):




Kwa mujibu wa Fromkin na wenzie (2007), Ishara 1 ilitumiwa kama pichataarifa kule Sumeria na baadaye ikabadilika kuwa Ishara 2 ya mfumo wa kikabari. Hata hivyo, ishara zote zilitumiwa ili kuwakilisha samaki.

**Mfumo wa Kihiroglifu**

Hiroglifu ni mfumo wa maandishi uliochipuka mwaka wa 3000KK kule Misri na ulitokana na athari za Wasumeria na Waakadia (Linguistic 203, h.t.). Mfumo huu ulihusisha ishara zilizotumiwa kuwakilisha konsonanti fulani. Konsonanti hizi ziliwakilishwa na michoro maalum ambayo ilifuatanishwa na hatimaye kuunda jambo husika. Baadhi ya ishara hizo ni kama zilivyodokezwa na Knight (2009:2), kama vile:

<u>**Picha**</u> <u>**Konsonanti**</u>




Mwandishi huweza kufuatanisha ishara moja baada ya nyingine ili kuunda neno maalum. Kuna hiroglifu za aina mbili: glifu ya kifonetiki ya kuwakilisha sauti za maneno na glifu ya kisemantiki ya

kuwakilisha maana za ishara (Knight, 2009). Mfumo wa kihiroglifu ulihusisha matumizi ya vifaa hasa mafunjo, poda iliyotengenezwa kutokana na mimea ya kuundia wino, burashi, na manyoya (Kasprowics, 2011). Vifaa hivi vilitumiwa ili kuchorea picha maalum zilizotumiwa kuwakilisha konsonanti husika.

**Mfumo wa Kilogografu**

Baada ya ishara kutumiwa katika mfumo wa kikabari na wa kihiroglifu kusimamia dhana na konsonanti, baadaye ishara hizi zilikuja kusimamia maneno (logografu). Hivyo basi, mfumo wa kilogografu hurejelea hali ambapo ishara hutumiwa kuwakilisha jina la kitu kuliko kitu chenyewe (Fromkin na wenzie, 2007). Katika mfumo kama huu, ishara ilitumiwa kuwakilisha neno na dhana dhahania. Mfumo wa kilogografu ulichipuka mwaka wa 2000KK kutoka kwa Wachina wakati ambapo pichataarifa zilitumiwa kama ishara za maneno (Linguistic 203, h.t.).

Ishara za kilogografu katika Kichina zilitumiwa ili kuwakilisha silabi, neno au maana mahususi (Norman, 1988). Kama vile, neno '*horse'* (farasi) liliwakilishwa kilogografu kwa kutumia ishara (馬) (ambayo ni ishara changamano) au ishara (马) (ambayo ni ishara sahili) (Norman, 1988:25). Ishara changamano ambayo ilitumiwa hapo awali na Wachina ilijumuisha michoro au alama nyingi zilizosumbua watu kuandika; hivyo basi, ishara sahili ilibuniwa yenye michoro au alama chache. Usahili kama huu wa ishara ulifanywa tu ili kurahisisha mafunzo ya maana za ishara husika.

Hivi sasa, mfumo wa kilogografu wa Kichina unaonekana kuathiri kwa kiasi kikubwa Kijapani ambacho kina mifumo minne ya uandishi kama vile *romaji* (ambapo herufi za Kirumi huwakilisha sauti za Kijapani), *hiragana* (hutumia mfumo wa kawaida wa kisilabi), *katakana* (kutokana na ishara za Kichina zilizotumiwa kuandika maneno yaliyokopwa) na *kanji* (inayotumia ishara za Kichina kuwakilisha maneno ya Kijapani) (www.english.illinois.edu/.../403/403 powerpoint/how.pdf)

**Mfumo wa Kisilabi**

Katika uandishi wa kisilabi, kila silabi iliwakilishwa na ishara maalum na kisha neno kuandikwa kwa kufuatanisha ishara za silabi hizo (Fromkin na wenzie, 2007; Yule, 1996). Kimsingi, katika uandishi wa kisilabi, silabi moja ilionekana ikisimamia labda wazo au jambo maalum (Gelb, 1963). Mfumo kama huu ulitumiwa zaidi kule Assyria

kama vile neno 'maatu' lenye maana ya kaunti liliandikwa kisilabi kama ifuatavyo (Fromkin na wenzie, 2007:509):




Hata hivyo, katika miaka ya 600-400KK, Waajemi walikuja kuvumbua njia nyingine rahisi ya kutumia uandishi wa kisilabi kama tunavyoona katika mfano ufuatao (Fromkin na wenzie, 2007:509):





**Mfumo wa Kialfabeti**

Ingawa majaribio ya binadamu kuhusu uandishi huweza kurejelewa nyuma zaidi ya miaka 20,000 iliyopita wakati michoro ilipochorwa kwenye mapango, maandishi yaliyokuwa na alfabeti huweza kurejelewa nyuma miaka 3,000 tu iliyopita (Yule, 1996). Uandishi wa kialfabeti humaanisha matumizi ya seti ya ishara zinazoweza kuandikwa ambazo aghalabu hutumiwa kuwakilisha sauti mahususi katika lugha (Yule, 1996). Ishara hizi hurejelewa moja kwa moja kama herufi za lugha ambazo hupangwa kwa utaratibu maalum katika maandishi (TATAKI, 2013).

Mfumo wa kialfabeti ulitamalaki hasa maandishi ya Kiebrania na Kiarabu (Yule, 1996) licha ya kuwa ulivumbuliwa na Wagiriki (Gelb, 1963). Mfumo wa kialfabeti ulitumiwa na Wagiriki kwa kuangazia vokali au irabu kama vile ***a*** (alpha) tofauti na konsonanti ***b*** (beta) (Yule, 1996). Mfumo huu wa uandishi wa kialfabeti hudhihirika hata katika lugha ya Kiswahili iliyo na herufi kama vile *b, ch, d, dh, f* (Kihore, Massamba & Msanjila, 2009) pamoja na lugha nyinginezo ulimwenguni. Maendeleo ya mfumo wa uandishi wa kialfabeti huweza kutazamwa katika dondoo ifuatalo (Yule, 1996:14) ambapo safu **A** huonyesha alfabeti za Kimisri, **B** (Kifonisi), **C** (Kigiriki) na **D** (Kirumi):

A B C D



Mfumo huu wa kialfabeti hasa wa Kirumi unaelezwa na Fromkin na wenzie (2007) kuwa unafaa zaidi katika sanaa ya uandishi. Ufaafu wake unatokana na sababu kuwa ni rahisi kufahamika, kutumiwa, na pia kunukuliwa (Fromkin na wenzie, 2007). Aidha, mfumo huu ni muhimu kwa sababu hudhihirisha hali ambapo sauti moja huwakilishwa na herufi moja ili kurahisisha maandishi ya lugha. Lugha nyingi ulimwenguni hutumia mfumo huu wa kialfabeti ambapo neno huundwa kutokana na alfabeti ambazo kimsingi hazina maana maalum zikiwa peke yake (Norman, 1988). Kama vile, '*a*' ni herufi tu au fonimu irabu ambayo haina maana maalum. Hata hivyo, herufi hii huweza kusimama peke yake au kufuatana na nyingine ili kuunda silabi ambazo pia hufuatana ili kuunda neno.

**Dhima za Sanaa ya Uandishi**

Sanaa ya uandishi ni mfumo ambao humfaidisha mno binadamu katika shughuli zake. Kwa mujibu wa Gelb (1963), sanaa ya uandishi huimarisha ustaarabu, maendeleo ya utamaduni na jamii na uvumbuzi wa vitu katika jamii. Uandishi husaidia pia ugunduzi wa utokeaji wa misimbo maalum katika lugha. Aidha, husaidia ugunduzi wa tofauti za kifonetiki kuhusu sauti fulani na tofauti za kimofolojia kuhusu neno baada ya kipindi maalum. Sanaa hii vilevile husaidia uimarishaji wa usanii ambapo wasanii husika hutumia mifumo na mitindo mbalimbali kuwasilisha ujumbe katika tungo zao. Katika tungo nyingi, uandishi hudhihirisha pia ujumisia maalum wa wasanii. Mathalani, maandishi ya kisheria, kibiblia na kimagazeti huzingatia ujumisia maalum wa kimtindo.

Sanaa ya uandishi hutumiwa katika mafunzo ya masuala ya kidini yaliyohifadhiwa katika maandiko matakatifu na kuweza kurejelewa kila mara. Mbali na hayo, uandishi hutumiwa kama ishara ya taifa kwa sababu mataifa huru huwa na makala maalum yaliyoandikwa kama vile katiba. Uharibifu wa turathi ya taifa huweza kutokea iwapo makala kuhusu taifa yataharibiwa na kuwaacha watu katika giza na hatimaye kukosa kujua walikotoka, waendako na stakabadhi zao muhimu zinazotumiwa kuendeleza shughuli za taifa.

Uandishi hutumiwa pia kuunganisha usemaji na maandishi. Hivyo basi, miundo iliyosemwa huweza kuhifadhiwa kimaandishi. Aidha, husaidia uhifadhi wa kumbukumbu za maneno ambayo hayajabwiwa ubongoni. Isitoshe, uandishi huhifadhi rekodi za matukio makubwa na mambo mengine yaliyotendeka katika jamii na mazingira husika. Katika kufanya hivyo, msomaji hupata muda wa kusoma maandishi

na hatimaye kupata kiini cha ujumbe ulioandikwa. Ujumbe kama huo huweza kutolewa pia katika makala nyingine ili kusaidia usambazaji wake.

**Mitindo Mbalimbali katika Sanaa ya Uandishi**

Ingawa kuna mifumo mbalimbali (taratibu za utendaji wa mambo fulani) ya uandishi, kama vile kikabari, kihiroglifu, kilogografu, kisilabi, na kialfabeti, watumiaji wa lugha huelekea pia kutumia mitindo (jinsi mahususi ya kufanya kitu kwa utaratibu fulani) katika mifumo hii ya sanaa ya uandishi. Jinsi hii ya kufanya kitu huonekana katika sanaa ya uandishi kama tunavyoona katika matumizi ya anagramu, kanuni ya rebasi, nadharia ya seti, emoji na akronimi ili kuwasilisha ujumbe kimaandishi.

Kuna mitindo kadha ya kuandika; kama vile kuandika kutoka kulia kwenda kushoto kama katika Kiarabu, kutoka juu kwenda chini kama Kichina, kutoka chini kwenda juu kama Kikaskajiani, na kutoka kushoto kwenda kulia kama vile lugha za Uropa na Kiafrika (Fromkin na wenzie*,* 2007). Hata hivyo, mtindo ambao umekolea mno katika lugha nyingi ulimwenguni ni ule wa kuandika herufi za maneno kutoka upande wa kushoto kwenda kulia huku herufi zenyewe zikipangwa kisilabi ili kuleta maana husika (Fromkin na wenzie, 2007). Mtindo huu aghalabu huonekana katika mfumo wa uandishi wa kialfabeti. Hata hivyo, kuna mitindo mingine midogomidogo ya kuwasilisha ujumbe katika mtindo huu wa kuandika kutoka kushoto kwenda kulia kama vile anagramu, kanuni ya rebasi, seti, emoji, na akronimi.

Mitindo hii yote huelekea kuonyesha hali ya kuchezea au kugeuza herufi, kutumia ishara, alama, ikoni au picha maalum na pia ufupisho wa maneno ili kuwasilisha ujumbe. Mitindo inayofafanuliwa katika makala haya si uvumbuzi mwingine wa sanaa ya uandishi bali ni njia nyinginezo za kuwasilisha ujumbe kimaandishi, hasa maandishi yale yanayozingatia mfumo wa kuandika kutoka kushoto kwenda kulia na wa kialfabeti. Huenda mitindo kama hii ya anagramu, kanuni ya rebasi, nadharia ya seti, emoji na akronimi hujitokeza pia miongoni mwa mifumo mingine ya uandishi kama vile kutoka juu kuja chini, kutoka kulia kwenda kushoto au hata kutoka chini kwenda juu. Hata hivyo, uchunguzi wa mifumo kama hiyo ya kuandika si dhamira ya makala haya.

**Anagramu**

Anagramu hufasiliwa kama neno, kirai au sentensi inayoundwa kwa kugeuza mpangilio wa herufi au silabi zake ili zisomeke kwa mfano kutoka mbele kurudi nyuma (Smith, 1980). Ni ubadilishaji wa herufi za neno husika ili kuunda neno lingine kwa kupangwa upya kama vile neno 'dame' linabadilishwa kuwa 'made' (Bussmann, 1996). Ubadilishaji wa mpangilio wa herufi unapofanywa basi uhusiano ufaao wa kimantiki huzingatiwa. Herufi za maneno husika pekee ndizo hugeuzwa. Hata hivyo, maneno yenyewe ambayo mpangilio wa herufi zake ziligeuzwa huendelea kuandikwa moja kwa moja kutoka kushoto kwenda kulia kama tunavyoona katika lugha nyingi ulimwenguni.

Encyclopaedia Britannica (1975) na Fromkin na wenzie (2007) wanaeleza kuwa matumizi ya awali ya anagramu huweza kurejelewa nyuma hadi kwa waandishi wa Kihibrania, kama vile Kabbalists, waliokuwa na mazoea ya kuchezea maneno tofauti na jinsi Kihibrania chenyewe kilivyoandikwa ili kuficha siri. Anagramu ilikita mzizi katika karne ya 16 na 17 BK na ilitumiwa pia na Warumi na Wagiriki na baadaye kusambaa hadi maeneo kadha ya nchi za Uropa (Encyclopaedia Britannica, 1975). Katika nchi ya Ufaransa, palikuwepo pia na mtaalamu aliyeitwa Thomas Billon aliyeteuliwa kuwa mwanaanagramu wa mfalme (Encyclopaedia Britannica, 1975).

Anagramu ilitumiwa katika shughuli za kidini hasa katika salamu maarufu za Kianjelika huku wanasayansi wengine, kama vile Christiaan Huygens, Robert Hooke, na Galileo, wakiitumia pia kama sitara ili kuficha matokeo ya tafiti zao ili wengine wasigundue na kuanza kudai uasili au nembo yake. Mwanzoni mwa karne ya 20 BK, baadhi ya waandishi walitumia mtindo wa anagramu ili kujipatia majina bandia ya kilakabu na katika kujazia mafumbo (Encyclopaedia Britannica, 1975).

Katika karne ya ishirini na moja, anagramu iliendelea kutumiwa kama tunavyoona katika fasihi. Mathalani, katika riwaya ya *Siku Njema*, mwandishi wa diwani ya *Malenga wa Bara* aliyetajwa katika riwaya hii amerejelewa kwa kutumia jina la kianagramu kama *Amuj Isokum* yaani *Juma Mukosi* (Mbatiah, 2001). Mtindo huu ulikuwa ubunifu wa mwandishi mwenyewe ili kuficha siri. Ubunifu huu ni dhihirisho kuwa, ingawa anagramu ni mtindo wa uandishi wa kale, mtindo huu ungali maarufu hasa katika ubunaji wa kazi za sanaa ili kuonyesha matumizi ya istilahi kimitindo.

Mtindo huu wa anagramu ulionekana pia miongoni mwa watoto Wahindi waliokuwa wakijifunza Kibengali ambapo silabi zake ziligeuzwa kutoka mbele kurudi nyuma kama vile neno *bisri* (sura mbaya) liligeuzwa kama *sribi* (Fromkin na wenzie, 2007). Japo waliyatumia maneno kama vile *bisri* na mengineyo katika mazungumzo, maneno hayo hayo yaliweza kuandikwa kwa sababu kile kinachosemwa na mtu huweza kuwakilishwa vilevile kimaandishi. Mifano tunayoweza kubuni katika Kiswahili kutokana na maelezo ya dhana ya anagramu ni kama vile:

| | | |
|---|---|---|
| ***Butaki*** | = | kitabu |
| ***Mulaka*** | = | kalamu |
| ***Mulimwa*** | = | mwalimu |
| ***Ritafda*** | = | daftari |

Hata hivyo lazima tung'amue kwamba anagramu hutofautiana na Sheng kwa kuwa Sheng inapobuni maneno maalum ya kumaanisha maneno mengine husika katika lugha wakati anagramu huelekea kubadilisha tu mpangilio wa silabi za maneno asilia bila kubuni misamiati mipya. Kuandika maneno kianagramu hakuonekani tu katika kategoria ya nomino pekee bali hujitokeza pia miongoni mwa kategoria nyingine. Hata hivyo, anagramu na Sheng huelekea kutumiwa katika uundaji wa sentensi. Maneno ya sentensi yenye kategoria mbalimbali hubadilishwa ama kwa kurejelea herufi au silabi. Tazama sentensi ifuatayo ya (i) ya Kiswahili sanifu na Sheng katika sentensi ya (ii) kama anavyodokeza Ogechi (2008:227):

i. Msichana Mkikuyu alimtaliki mvulana Mluhya. (Kiswahili sanifu).
ii. Dem msapere alimtema chali Mlunje. (Sheng)

Sentensi (i) ya Kiswahili sanifu ikiandikwa kianagramu basi huonekana kama ifuatayo katika sentensi (iii):

i. Nachasim yukukim kilitamlia nalavum yahlum. (Anagramu)

Ingawa ni vigumu kutambua maneno ya Sheng kwa wale wasioizoea, kwa upande mwingine ni rahisi kugundua lugha asilia ya sentensi za anagramu husika kutokana na matumizi ya maneno ya palindromu. Palindromu humaanisha neno linaloweza kusomeka kwa namna moja ama kwa kawaida kwenda mbele au kurudi nyuma bila kupoteza umbo asilia (TUKI, 2000). Palindromu huonekana miongoni mwa

maneno kama vile ama, ana, utu, omo, ili, ini na kadhalika ambayo hayabadiliki kimuundo yakiandikwa kianagramu. Kutokana na hali ya kutobadilika kwa miundo ya maneno ya palindromu, wataalamu wengine huidhukuru kama aina spesheli ya anagramu ambapo maneno yake yanaweza kusomeka sawasawa ama kwenda mbele au kurudi nyuma (Encyclopaedia Britannica, 1975).

Simo hii ya anagramu hujitokeza aghalabu miongoni mwa wanajamii anuwai na hasa katika maeneo ya mashambani. Mathalani, katika lugha ya Kiluo, kuna anagramu inayoitwa kama '*Dho-Chi'* (Borowsky & Avery, 2009). Baadhi ya matumizi yake katika Kiluo ni kama vile:

| | | |
|---|---|---|
| ***Nanga*** (nguo) | = | *ngana* |
| ***Chak*** (maziwa) | = | *kach* |

Mtindo huu hautumiwi tu na watu katika usemi pekee ili kuficha siri bali hutumiwa pia na watu husika wanapoandika ujumbe huo wa siri kianagramu. Hivyo basi, anagramu ni mtindo ambao haujitokezi tu katika usemi pekee bali pia maandishi. Shuruti tukumbuke kuwa maandishi aghalabu ni mtindo tu wa kuhifadhi kile ambacho huweza kusemwa.


**Kanuni ya Rebasi**

Kanuni ya rebasi inamaanisha hali ambapo ishara maalum zinatumiwa kwa minajili ya kuwakilisha sauti ya lugha badala ya kitu chenyewe halisia (Encyclopaedia Britannica, 2016; Rebus Game, h.t.; Frazer, 2011). Kimsingi, kanuni hii inahusisha matumizi ya pichataarifa kwa kurejelea thamani ya sauti yake (Fromkin na wenzie*,* 2007). Hivyo basi, kanuni ya rebasi ni hali ya kuwakilisha maneno na picha za viumbe ambavyo majina yake hutoa sauti kama neno husika linalorejelewa (Frazer, 2011).


Mtindo kama huu ulitumiwa kule Misri katika mfumo wa kihiroglifu na hata mapema katika miaka ya 3400KK (Frazer, 2011). Mifano yake ni kama vile picha ya jicho huwakilisha dhana ya kiwakilishi 'I', picha ya nyuki huwakilisha dhana ya silabi {be} na picha ya tawi huwakilisha mofu {leave}. Kwa jumla, rebasi ya Kiingereza inayoundwa kutokana na mofu hizo ni kama vile '*I believe'.* Fungu hili kimsingi halina uhusiano wowote na 'eyes', 'bees' na 'leaves' (Frazer, 2011). Tazama jinsi fungu hili la '*I-be-lieve*' linavyoonyeshwa kwa kutumia mfumo wa rebasi (Fromkin na wenzie, 2007:510) kama vile:




Vilevile katika rebasi ya Kiingereza, neno ‘idea’ yaani wazo huweza kuwakilishwa kwa njia ya rebasi kama ifuatayo (Frazer, 2011:1):




Maneno kama vile ‘*I see you’* huweza kuwakilishwa kwa mtindo wa rebasi ya Kiingereza kama anavyodhihirisha Frazer (2011:1), kama vile:




Maneno kama vile ‘eye’ /aI/ au kiwakilishi nafsi ‘I’ /aI/ hutamkwa kwa namna inayofanana licha ya kwamba huandikwa kwa jinsi tofauti. Aidha, ‘*sea*’ /si:/ na ‘*see*’ /si:/ vilevile hutamkwa kwa namna inayofanana (Hornby, 2010). Inabainika kuwa ni vigumu kutumia kanuni ya rebasi katika lugha nyingi ikiwemo Kiswahili. Hii ni kwa sababu maneno chungu nzima ya Kiswahili huelekea kuandikwa jinsi yanavyotamkwa tofauti na maneno mengine ya Kiingereza. Inajitokeza kuwa kanuni ya rebasi huonekana miongoni mwa maneno machache tu ya lugha kama tunavyoona katika Kiingereza. Umuhimu wa kanuni ya rebasi ni kwamba inaweza kutumika katika masuala ya vitendawili, matangazo na hata vichekesho au dhihaka (Fromkin na wenzie, 2007). Uandishi wa aina hii husaidia kuonyesha picha pamoja na maneno ili kurahisisha maana ya kile kinachorejelewa.

## Matumizi ya Nadharia ya Seti

Borschev na Partee (2001) wanaeleza dhana ya seti kama mkusanyiko wa vipashio husika katika kundi maalum. Vipashio hivi vinaweza kuwa watu, vitu, nambari, ishara na hata wanyama. Vitu hivi vinavyowekwa katika seti aghalabu huunda chama au kundi maalum

linaloundwa kwa kufuata ruwaza ifaayo. Hivyo basi, vitu hivyo hudhukuriwa moja kwa moja kama wanachama wa seti husika walio na sifa bainifu (Stephan, 2009). Kimsingi, nadharia inayochunguza vipashio vinavyojumuishwa katika seti husika hurejelewa moja kwa moja kama nadharia ya seti (Enderton, 1977).

Nadharia ya seti hutumiwa katika taaluma za hisabati, isimu na filosofia (Enderton, 1977). Ingawa nadharia ya seti inahusisha nambari katika hisabati, seti inaweza pia kutumiwa kuonyesha uhusiano kati ya seti za sentensi zinazounda usemi (Bonissone, 1980) na seti za fahiwa za leksimu za lugha husika. Mathalani, sentensi yoyote ile ya lugha kimsingi huwa na seti za makundi mawili: kundi nomino (KN) na kundi tenzi (KT). Kwa mfano, usemi 'Mwanafunzi hodari anasoma kitabu' hudhukuriwa kama seti kuu inayojumuisha seti mbili za KN (Mwanafunzi hodari) na KT (anasoma kitabu). Fahiwa mojawapo inayoweza kufafanuliwa kwa kutumia nadharia ya seti ni hiponimia ambayo inaonyesha uhusiano baina ya leksimu jumuishi (hipanimu) na leksimu mahususi (hiponimu) kama tunavyoona katika fahiwa ya rangi (Cruse, 1986; Enderton, 1977). Kwa mfano, seti kuu ya rangi hujumuisha rangi mahususi kama vile -ekundu na -eupe.

Vipashio vya nadharia ya seti huweza kuwasilishwa kimaandishi kwa kuzingatia alama maalum ya Kigiriki inayoitwa epsiloni (∋) (Hornby, 2010). Alama hii huweza kuandikwa kwa kuzingatia mifumo miwili: (∋) na (∈) (Benz, Jager & van Rooij, 2007; Chen, 1999; Roitman, 2011; Stephan, 2009; Weiss, 2008). Mfumo wa kwanza wa epsiloni (∋) humaanisha kijumuishi na mfumo wa pili wa epsiloni (∈) hurejelea vijumuishwa vya kundi fulani. Mfumo wa kwanza wa matumizi ya epsiloni ni kama vile: A ∋ {1, 2, 3, 4...} yenye maana kuwa seti {A} hujumuisha vipashio {1, 2, 3, 4...}. Mfumo wa pili wa matumizi ya epsiloni hurejelea dhana ya vijumuishwa kama vile: {1, 2, 3, 4...} ∈ {A} unaomaanisha kuwa vipashio hasa {1, 2, 3, 4...} hujumuishwa katika seti kuu inayojulikana kama {A}.

Kuna njia maalum inayotumiwa kuwasilisha kimaandishi vipashio vya seti kama vile kufunga vipashio katika mabano { } na kutenganisha vipashio hivyo kwa kutumia alama ya mkato (,) (Borschev & Partee, 2001). Matumizi ya alama hizi katika nadharia ya seti huweza kudhihirika katika mifano ifuatayo ya kutumia maneno katika isimu kama vile: **Chakula** ∋ {ugali, nyama, samaki, mboga}. Mfano huu una maana kuwa seti kuu yaani 'chakula'

hujumuisha vipashio au elementi kama vile {ugali, nyama, samaki, mboga}. Mfumo wa pili wa epsiloni wa kuonyesha kuwa vipashio au elementi za dhana fulani huweza kuangaziwa kwa mujibu wa nadharia ya seti kama vile: {Ugali, nyama, samaki, mboga} ∈ **Chakula.**

Kinachodhihirika hapa ni kuwa licha ya sanaa ya uandishi kuelekea kuegemea mno matumizi ya herufi kama ishara, pia kuna matumizi mengine ya alama hasa epsiloni na mabano ili kuwasilisha wazo maalum kimaandishi na kwa njia ya ufupisho. Hivyo basi, badala ya kutumia maneno mengi kurejelea suala kama vile 'chakula kinajumuisha hiponimu mahususi kama vile ugali, nyama, samaki na mboga', tunaweza kufupisha fungu hili kama vile: **chakula** ∋ {ugali, nyama, samaki, mboga}.

**Matumizi ya Emoji**

Emoji ni mtindo ambapo picha au ishara maalum hutumiwa kuwasilisha ujumbe (Kelly, 2015) na mtindo huu mwanzoni ulichipuka kule Japani (Oxford University Press, 2016). Emoji huundwa kutokana na herufi 'e' na 'moji' (Merriam Webster Incorporated, 2015). Herufi 'e' hurejelea picha na 'moji' hurejelea herufi au ujumbe maalum (Merriam Webster Incorporated, 2015). Hivyo basi, emoji ni picha zinazotumiwa kuwasilisha ujumbe maalum.

Emoji hudhukuriwa kama mfumo mojawapo wa pichataarifa ambao ulianza kuonekana katika miaka ya 1990 (WGSN, 2015) kutokana na shughuli za kampuni ya mawasiliano ya simu ya Kijapani hasa *NTT DoCoMo* na *SoftBank Mobile* (Vodafone) (Ogeto, 2015). Kama mfumo mojawapo wa pichataarifa, emoji huonyesha picha zenye maana zinazojulikana na watumiaji wake. Picha hizi huweza kutumiwa peke yake au kwa kuambatanisha na maneno katika uwasilishaji wa ujumbe.

Kabla ya kuchipuka kwa emoji, kulikuwepo pia na emotikoni iliyoundwa kutokana na kufupishwa kwa maneno hasa 'emotional icons' (ikoni za kihisia) zilizotumiwa kuonyesha hisia tu (Kelly, 2015). Tofauti ni kwamba emotikoni inapoonyesha hisia pekee yake, emoji huelekea kuonyesha hali nyinginezo kama vile hisia za nyuso, ishara za siku kuu, matukio, wanyama na kadhalika (Kelly, 2015). Emoji ilitokana na seti za ikoni zilizobuniwa na mtu aliyeitwa Shigetaka Kurita mnamo mwaka wa 1995 (Pelegrin, 2014, katika Kelly, 2015). Msambao wa emoji ulionekana kule Asia hasa katika kicharazio cha simu.

Baadhi ya ishara za emoji zinamaanisha mambo kama vile furaha, tabasamu kubwa, utulivu, hisia nzuri, uchungu, woga wa kupindukia, ugonjwa, hasira kubwa, upendo na hata kuvunjika kwa upendo (Ogeto, 2015). Ikoni za emoji zinazotumiwa ni kama vile za uso usio na furaha, picha ya ujauzito, picha ya mtu anayecheza, picha za mparachichi, karoti, viazi, mtango na picha za wanyama na ndege kama vile popo, bundi, tai, bata na hata papa (Emoji subcommittee, 2015). Tazama mifano ya picha zifuatazo za emoji na maana zake (NikiSelken, 2016) katika Jedwali 1:

**Jedwali 1: Mifano ya Ikoni za Emoji na Maana zake**

| Ikoni ya Emoji | Jina | Maana |
|---|---|---|
|  | Moyo | Upendo, mapenzi |
|  | Moyo, macho, uso | Kuona mapenzi, kukubali |
|  | Midomo/vimidomo | Tabasamu, mazungumzo, kubusu |
|  | Miwani | Kuona |
|  | Uso unaolia | Huzuni |
|  | Mikono miwili iliyoambatanishwa | Omba, shukuru |

Ingawa matumizi ya emoji yanaelekea kuwa na natija maridhawa miongoni mwa watu, mtindo huu una dosari katika jamii. Mathalani, ripoti ya Jenna Wortham katika *Womanzine's Emoji Issue* inaonyesha hofu kwamba huenda kufikia miaka ya 2115 lugha 600 pekee zitasalia kati ya zaidi ya lugha 6000 zinazotumiwa hivi sasa ulimwenguni (WGSN, 2015). Hali hii huenda ikatokea kwa sababu ya matumizi ya kila mara ya mtindo wa emoji miongoni mwa vijana yanayoimarishwa na mfumo mpya wa kidijitali katika mawasiliano. Hata hivyo, hii ni hofu tu ambayo haiwezi kudhihirika kwa sababu matumizi ya emoji huchukua nafasi finyu sana katika mawasiliamo ulimwenguni na mambo yote hayawezi kuwasilishwa kwa mtindo wa emoji.

Aidha, ripoti ya *PewReportCentre* iliyotolewa December 2011 inadhihirisha kuwa vijana wa huko Marekani huelekea kuwasiliana zaidi kwa kutumia matini ikifuatwa na mtandao wa kijamii kuliko njia nyinginezo (*PewReportCentre*, 2016). Mbali na hayo, utafiti wa 2014 wa kampuni ya *TakTalk Mobile* ya Uingereza ulidhihirisha vilevile kuwa watu wanane kati ya kumi ulimwenguni wamewahi kutumia ishara na ikoni ili kuwasiliana (Ogeto, 2015). Katika kuimarisha mawasiliano miongoni mwa vijana na watu wazima kwa kutumia matini, kumetokea mtindo wa kutumia ishara za emoji (WGSN, 2015). Hivi sasa emoji huweza kudhukuriwa kama 'lugha ya dunia' nzima inayotumiwa na watu ulimwenguni hasa katika mawasiliano ya kisasa ya kidigitali (WGSN, 2015). Mathalani, mnamo mwaka wa 2014 picha ya 'moyo' ilitumiwa zaidi katika mawasiliano miongoni mwa watu wengi duniani kote kuonyesha upendo (WGSN, 2015). Picha hiyo ilionyeshwa kama ifuatayo:



**Kielelezo 1: Ikoni ya Moyo ya Kuonyesha Upendo**
(WGSN, 2015:5)

Ingawa emoji inadhukuriwa kama 'lugha' katika makala mbalimbali, mnamo Disemba 13 mwaka wa 2015 mwanaisimu aitwaye Neil Cohn alitahadharisha kuwa emoji inaweza kushindana na Kiingereza ulimwenguni. Hata hivyo, haiwezi kuitwa lugha kwa sababu haina sarufi. Hivyo basi, kile kinachodhihirika ni kipengee kimoja tu kuhusu maana (BBC, 2016). Ishara au ikoni hizi za emoji zinaweza kufuatana ili kuwasilisha ujumbe; hata hivyo, hali hiyo haimaanishi kuwa ni lugha mpya inayovumbuliwa. Emoji imewahi kutumiwa katika mahakama kama ushahidi katika nchi za ng'ambo, kutumiwa katika sanaa kama vile Emoji Art Gallery, Emoji Art & Design Show, Emoji Haiku na Emoji Dick (WGSN, 2015). Mifano zaidi ya matumizi yake huonekana katika matangazo ya kampuni ya *Coca-Cola* kuhusu soda ya *coke* ambayo inatangazwa kama *Coca Cola Emoti Coke* kama tunavyoona katika picha ifuatayo:




**Kielelezo 2: Tangazo la Kampuni ya Coca Cola kuhusu Coke**
(WGSN, 2015:7)

**Matumizi ya Akronimi**

Akronimi ni mtindo maalum unaotumiwa na wanaisimu ili kuunda istilahi mbalimbali yaani akronimu katika lugha yoyote husika. Kwa upande mwingine, akronimu humaanisha neno lolote linaloundwa kutokana na herufi za mwanzo za majina husika (TATAKI, 2013), kwa mfano, TATAKI huwakilisha Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. Aghalabu, herufi hizi za mwanzo za maneno hufaa kuandikwa kwa njia ambayo zinaweza kutamkika kama vile VIP (Very Important Person) (Laili, 2008).

Akronimu haina mfumo mmoja shikilizi wa uundaji wake (Briton, 2000, katika Laili, 2008). Hivyo basi, kuna mfumo wa kuchukua herufi mbili za mwanzo katika neno ili kuweza kutamkwa kama vile BAKITA (Baraza la Kiswahili la Taifa) na mfumo wa kuruka neno au maneno mengine wakati wa uundaji wa akronimu (Laili, 2008). Aidha, akronimu huweza kudhihirika kama vifupisho ambavyo haviwezi kusomeka lakini husimamia dhana maalum kama vile CSE (*Certificate of Secondary Education*), EC (*European Community*) na DDP (*Director of Public Prosecution*) (Katikiro, 2014:37).

Hivi sasa, vijana wanaelekea kutumia mtindo wa kuchanganya emoji pamoja na akronimu katika maandishi yao. Hivyo basi, wanatuma ujumbe ulio na picha zile za emoji pamoja na akronimu husika. Kwa mujibu wa Ogeto (2015:2), baadhi ya akronimu wanazotumia vijana hivi sasa ni kama vile:

| **Akronimu** | **Kirefu chake** |
|---|---|
| **UPY** | Uko peke yako |
| **PAW** | parents are watching |
| **CU46** | see you for sex |
| **FWB** | friends with benefits |

| | |
|---|---|
| **HNK** | hugs and kisses |
| **IDK** | I don't know |
| **T2UL** | talk to you later |
| **TU** | thank you |
| **GNOC** | get naked on cam |
| **2D** | to day |
| **TDTM** | talk dirty to me |
| **PTB** | please text back |
| **4EAE** | for ever and ever |
| **FTF** | face to face |
| **NM** | never mind |
| **WTPA** | where the party at |
| **WYCM** | will you call me |
| **MOS** | mom over shoulder |
| **RUK** | are you okay |

Kinachodhihirika hapa ni kuwa akronimu nyingi zinaelezwa kwa kutumia Kiingereza. Hata hivyo, kuna mifano mingine ambayo inatumia Kiswahili kama vile: **UPY** (uko peke yako). Mbali na mfano huu, kuna pia matumizi ya tarakimu kama vile **2D** (to day), **7bu** (sababu) na **muhi2** (muhimbili). Hivyo basi, matumizi ya akronimu hizi hudhihirisha hali ya kuchanganya ndimi kama vile Kiingereza na Kiswahili, na tarakimu. Mifano ya maandishi yanayohusisha matumizi ya akronimi hizi katika sentensi ni kama vile:

'**UPY** **2D** ama **PAW**. Can **I T2UL**. **PTB**. **TU**'

Fungu hili linaweza kuelezwa kwa kutumia maneno kama vile: *Uko peke yako to day* ama *parents are watching*. Can I *talk to you later*. *Please text back*. *Thank you*.

**Hitimisho**

Makala haya yamedhihirisha kuwa kuna mitazamo anuwai kuhusu chimbuko la sanaa ya uandishi. Uvumbuzi wa sanaa ya uandishi ulichipuka hasa baada ya binadamu kujua kutumia lugha na ulichochewa na hali ya kutaka kuweka rekodi za vitu alivyohodhi na kuweka kumbukumbu za matukio katika mazingira yake. Hivyo basi, binadamu alianza kutumia malighafi zilizokuwepo karibu ili kujichorea ishara zilizotumiwa katika mawasiliano. Ishara hizi zilikuja kurejelewa kama pichataarifa na wazotaarifa. Baadaye mifuatano ya maendeleo ya mifumo ya sanaa ya uandishi ikawa: kikabari, kihiroglifu, kilogografu, kisilabi na kialfabeti. Mfumo wa kialfabeti ndio umetamalaki uandishi wa lugha nyingi ulimwenguni.

Hata hivyo, lugha nyingi zinazotumia mfumo huu wa kialfabeti huelekea kudhihirisha vilevile mitindo mingine mbalimbali ya maandishi au michezo ya lugha kama tunavyoona katika anagramu, nadharia ya seti, kanuni ya rebasi, emoji na akronimi hasa katika mawasiliano ya kisasa.

Inabashiriwa kuwa kutokana na hali ya kupendelea ishara anuwai katika mawasiliano kutokana na maendeleo ya kidigitali, kuna hofu kuwa huenda zile lugha tunazotumia hivi sasa ulimwenguni zikapungua kwa kiwango fulani. Hali kama hiyo ikitokea basi huenda tutarudia tena matumizi ya zamani ya pichataarifa na wazotaarifa katika mawasiliano. Tayari matumizi kama hayo yanaonekana katika emoji, akronimi na hata mfumo wa nadharia ya seti.

## Marejeo


Amanda, L. (2015). *Theories of Language Origin.* Kinapatikana katika: https://etimology.wikispaces.com/Theories+of+Language+Origin

Baroni, A. (2011). Alphabetic vs Non-alphabetic Writing: Linguistic Fit and Natural Tendencies. *Rivista di Linguistica*, 23(2): 127–159. Yanapatikana katika: https://www.academia.edu/702320/Aphabetic_Vs_Non_Alphabetic_Writing_Linguistic_Fit_and_Natural_Tendencies

BBC. (2016). *Will Emoji Become a New Language*? Kinapatikana katika: http://www.bbc.com/future/story/20151012-will-emoji-become a-new-language

Benz, A., Jager, G. & van Rooij, R. (2007). *An Introduction to Game Theory for Linguists*. Kinapatikana katika: http://www.web.mit.edu/linguistics/events/iap07/Benz-Jager-vanRooy.pdf

Bible Society of Kenya. (1997). *Biblia*. Nairobi: Bible Society of Kenya.

Bonissone, P. P. (1980). A Fuzzy Set Based Linguistic Approach: Theory and Applications. *Proceedings of the 1980 Winter Simulation Conference*, 99–111. Yanapatikana katika: www.people.vcu.edu/~lparker/DBGroup/References/Theory.pdf

Borowsky, T, & Avery, P. (2009). Dhochi: A Dholuo Language Game. *Australian Journal of Linguistics*, 29(2): 169–194. Yanapatikana katika: http://sydney.edu.au/arts/linguistics/images/content/staff/Borowsky_Avery_2009.pdf

Borschev, V., & Partee, B. (2001). Lecture 1. Basic Concepts of Set Theory. *Ling 726: Mathematical Linguistics*, September 6: 1–

6. Yanapatikana katika: http://www.people.umiss.edu/Partee/726_01/lecture/lecture1.pdf

Bussmann, H. (1996). *Routledge Dictionary of Language and Linguistics*. London: Routledge.

Chen, R. (1999). The Categorization and Taxonomy of Scientific Theories. *11th International Congress of Logic, Methodology and Philosophy of Science*. Yanapatikana katika: www.scu.edu.tw/Philos/Index/teacher/Chen/Microsoftword-Categorization and Taxonomy.pdf

Cheng, L. (h.t.). *The Evolution of English Writing System: A Review of Spelling Reform*. Kinapatikana katika: http://reserach.ncl.ac.uk/ARECLS/volume_4/Cheng.pdf

Cruse, D. A. (1986). *Lexical Semantics*. Cambridge: Cambridge University Press.

Emoji Subcommittee (2015). *Emoji Additions: Animals, Compatibility, and More Popular Requests.* Kinapatikana katika: http://www.unicode.org/L2/L2015/15054r4-emoji-tranche5.pdf

Enderton, H. B. (1977). *Elements of Set Theory*. New York: Academic Press. Kinapatikana katika: www.math.ucla.edu~hbe/ency.pdf

Encyclopaedia Britannica. (1975). *The New Encyclopaedia Britannica*. (Volume 1). USA: Encyclopaedia Britannica Inc.

Encyclopaedia Britannica. (2016). *Rebus Writing Principle*. Kinapatikana katika: https://www.britannica.com/topic/rebus-Writing-Principles

Falck, K. (2001). *The Practical Application of Pictogram*. Kinapatikana katika: http://static.pictosys.se/pictogram/practicalapp_pictogram.pdf

Frazer, D. (2011). *The Rebus Principle.* Kinapatikana katika https://egyptologyman.wordpress.com/2011/02/17/the-rebus-principle/trackback/

Fromkin, V., Rodman, R., & Hyams, N. (2007). *Introduction to Language*. USA: Thomson Wadsworth.

Gelb, I. J. (1963). *A Study of Writing*. Kinapatikana katika: www.oi.uchicago.edu/Sites/oi.uchicago.edu/files/uploads/shared/docs/study_writing.pdf

Hornby, A. S. (mh.) (2010). *Oxford Advanced Learner's Dictionary* (toleo la 8). Oxford: Oxford University Press.

Kasprowics, D. (2011). *The History of Writing: Introduction to the 7th Language Arts Programme.* Kinapatikana katika: www.orias.berkeley.edu/mapping/Scripts/HistoryofWriting.pdf

Katikiro, E. G. (2014). Lemma or No Lemma? Dislocation of Acronyms in Kiswahili Lexicography. *Jarida la Kiswahili*, 77: 23–40.

Kelly, C. (2015). *A Linguistic Study of the Understanding of Emoticoms and Emojis in Text-Messages*. Kinapatikana katika: http://www.diva-portal.org/smash/get/diva2:783789/FULLTEXT01.pdf

Kihore, Y. M., Massamba, D. P. B. & Msanjila, Y. P. (2009). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu (SAMAKISA): Sekondari na Vyuo*. (Chapa ya 5). Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Knight, S. C. (2009). *Egyptian Writing System and Grammar.* Kinapatikana katika: www.andrew.cmu.edu/course/98-030/Writing.pdf

Laili, N. M. (2008). *A Study of Onomatopoeia in Vatar Comic*. Kinapatikana katika: www.lib.uin.Malang.ac.id/files/thesis/fullchapter/04320092.pdf

Linguistic 203. (h.t.). *Writing.* Kinapatikana katika: http://udel.edu/~dlarsen/ling203/slides/writing.pdf

Mbatiah, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Standard Textbooks Graphics and Publishing.

Mentalfloss. (2016). *6 Early Theories About the Origin of Language*. Kinapatikana katika: http://mentalfloss.com/article/48631/6-early-Theories-about-origin-language

Merriam Webster Dictionary (2015). *Origin of Emoji.* Inapatikana katika: http://www.Merriam-Webster-com/dictionary/emoji

Selken, N. (2016). *The Emoji Dictionary*. Inapatikana katika: http://emojidictionary.emojifoundation.com/home/home.php?emoji=emoji109.jpg

Norman, J. (1988). *Traditional and Transformation in the Chinese Writing System.* Kinapatikana katika: http://www.sites.asiasociety.org/education/VISIBLETRACES/curriculum/pdf/CIAessay1.pdf

Ogechi, N. O. (2008). Kiswahili Kina Mchango Gani katika Sheng? Katika N. O. Ogechi, N. L. Shitemi & K. I. Simala (wh.). *Nadharia katika Taaluma ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika*. Chuo Kikuu cha Moi: Moi University Press, 227–39.

Ogeto, A. (2015). Expressive and Cheecky: the Language of Emoji Looks into the Future. *Daily Nation, DN2,* Wednesday, September 1–2. Nairobi: Nation Media Group Ltd.

Olson, D. R. (2009). *The History of Writing*. Kinapatikana katika: http://www.sagepub.com/sites/default/files/upmbinaries/27267_5276_Bearad_ch01.pdf

Oxford Univerity Press. (2016). *Oxford Dictionaries. Language Matters*. Zinapatikana katika: http://www.oxforddictionaries.com/definition/english/emoji

Pew Report Centre. (2016). *Texting, Social Networking, Popular Worldwide*. Kinapatikana katika: http://www.pewresearch.org/topics/texting/pages/3/

Rebus Game (h.t.). *Rebus Principle. Historic Example*. Kinapatikana katika: www.usc.edu/dept/LAS/arc/games/rebusex.htm

Roitman, J. (2011). *Introduction to Set Theory*. Kinapatikana katika: www.math.ku.edu/~roitman/Stb3fullWeb.pdf

Smith, A. H. (1980). *The Encyclopedia Americana*. USA: Danbury Connecticut Grolie.

Sprunger, D. (h.t.). *Theories of Language Origin*. Kinapatikana katika: www.faculty.cord.edu/Sprunger/e315/languageorigins.pdf

Stephan, F. (2009). *Set Theory*. Kinapatikana katika: www.compo.nus.edu.sg/~fstephan/settheory.pdf

TATAKI. (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (Toleo la 3). Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.

The Huntington Library (h.t.). *Development of Writing and Books. Part II.* Kinapatikana katika: www.huntington.org/uploadFiles/Files/PDF/LHPPPwritingbooks2.pdf

Thompson, I. (2016). *Writing Systems*. Kinapatikana katika http://aboutworldlanguages.com/writing-systems

TUKI. (1990). *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: TUKI.

TUKI. (2000). *English-Swahili Dictionary.* Dar es Salaam: TUKI.

WGSN. (2015). *Without Words: Emoji Solutions*. Kinapatikana katika: http://www.Wgsn.com/assets/Marketing/emails/2015

Weiss, W. A. R. (2008). *An Introduction to Set Theory*. Kinapatikana katika: http://www.math.toronto.edu/weiss/Set_Theory.pdf

Yule, G. (1996). *The Study of Language* (Toleo la 2). Cambridge: Cambridge University Press.